



**USAID**  
FROM THE AMERICAN PEOPLE

Christian Social Services Commission (CSSC)



# Workshop Bulletin

## Sekta binafsi inamchango mkubwa katika Sekta ya Afya

IMEELEZWA kuwa sekta binafsi inamchango mkubwa katika sekta ya afya endapo ushirikano baina ya watoa huduma binafsi, makanisa na Serikali utazidi kuimarika.

Akizungumza katika mkutano wa siku mbili uliyowakutanisha wadau wa sekta ya afya, Mkurugenzi wa Tume ya Kikristo za Huduma za Jamii (CSSC) Dkt. Adeline Kimambo amesema ushirikiano uliyopo baina ya Serikali na Sekta binafsi ni mzuri, ambapo kwa sasa Serikali kupitia baadhi ya halmashauri za wilaya zimeanza kuajili watumishi na kuwapeleka kwenye hospitali zinazomilikiwa



na Taasisi za dini ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa watumishi ambalo kwa sasa ni kubwa katika hospitali hizo. Aidha katika kutekeleza azima ya ushirikiano huo unaojulikana kama Public Private Partnership (PPP), Dkt. Kimambo ameeleza kuwa tayari kuna vituo 7 vya afya vinavyomilikiwa na makanisa vimesaini mkataba wa utoaji huduma ya afya na halmashauri za wilaya hali ambayo itapelekea huduma hiyo kuimarika, na kutoa wito kwa halmashauri zingine kuingia katika mpango huo.

Katika hatua za kukabiliana na tatizo hili, CSSC kwa kushirikiana na shirika lingine la Intrahealth kwa ufadhili wa shirika la misaada la marekani (USAID), imeanzisha mradi wa Rasilimali watu ambao unaainisha na kutambua idadi ya watumishi, kada, na elimu zao.

Naye mratibu wa mradi huo Bw. Petro Pamba amesema kuwa mkutano huo umelenga kuboresha matumizi ya Sera na Miongozi iliyopo ya Rasilimali watu katika Sekta ya Afya, kutambua mahitaji ya watumishi yanayotakiwa ili kuwajengea uwezo kwa kuwaendeleza. Bw Pamba amesema mfumo wa Rasilimali watu unatumika

kutunza takwimu za watumishi kwa njia ya Mtandao wa Kompyuta hivyo inakuwa rahisi kwa hospitali kujua idadi



ya watumishi iliyonao, kada na elimu zao.

Awali akifungua mkutano huo, kwa niaba ya Katibu mkuu wa Baraza la maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Musinyori Julian Kagalawe, amesema makanisa yamekuwa mstari wa mbele katika kutoa huduma ya afya nchini ambapo mafanikio yanaonekana kutokana na huduma nzuri itolewayo na hospitali za rufaa za Bugando na KCMC zinazomilikiwa na makanisa.

Pamoja na hayo Musinyori Kagalawe amesema kuwa hivi sasa nchi inauhaba wa rasilimali watu 32,000 ambayo ni sawa na asilimia 61, huku takwimu za hivi karibuni zikionyesha kuwa nchi ina madaktari 1339 pamoja na wale wa kwenye sekta binafsi 455, hivyo kufanya daktari 1 kuhudumia wagonjwa 25,000.

Tume ya Kikristo ya huduma za jamii (CSSC) ni chombo cha pamoja kati ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) na Baraza la Kikristo Tanzania (CCT) kilichoundwa mwaka 1992 kwa lengo la kusaidia huduma za jamii kwa upande wa Afya na Elimu kupitia hospitali na shule zinazomilikiwa na makanisa.



Habari na : Renatus Sona  
Rachel Mkundai  
Picha na layout: Renatus Sona



**INTRAEALTH**  
INTERNATIONAL